# BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 27 Mei, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kwa Mwaka 2021/2022.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kwa Mwaka 2021/2022.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

121. MHESHIMIWA HABIB ALI MOHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kwa kuwa Zanzibar ni nchi maskini ambayo inahitaji misaada kutoka kwa wadau mbali mbali duniani. Na kwa kuwa misaada mingi huwa na athari ya kisheria.

(a) Je, Serikali inasemaje juu ya uwezo na athari za kisheria katika kuingia mikataba na uanachama katika Mashirika ya Kimataifa.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuipigania Zanzibar kujiunga katika Shirika la OIC ambalo litaweza kuisaidia Zanzibar katika kukuza uchumi wake.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

152. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MANDOBA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali imefanya jambo bora kwa kuamua kuwapeleka vijana wetu JKU na JKT wanapomaliza masomo ili kupata mafunzo ya uzalendo wa nchi yao na pia kuacha kukaa bure vigengeni na kufikiria mambo maovu.

(a) Je, ni muda gani vijana wale wanakaa makambini na nini lengo la Serikali baada ya kutoka makambini vijana wale.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia ajira wale wote waliomaliza mafunzo hayo.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

194. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Upatikanaji wa huduma ya umeme katika miji na vijiji unasaidia sana katika kuinua hali ya wananchi. Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) limepunguza gharama za kuunganisha umeme kutoka laki nne (400,000/) mpaka kufikia laki mbili (200,000/-). Hata hivyo, wananchi wenye kipato cha chini bado wanaona kuwa gharama hiyo ni kubwa.

(a) Je, Shirika linawaangalia vipi wananchi wa kipato cha chini kuwapatia punguzo maalum ili kumudu gharama za kuunga huduma ya umeme.

(b) Kuna utaratibu gani utakaowasaidia wananchi wa kipato cha chini kuweza kumudu gharama za umeme mara baada ya kujiunga na huduma hiyo.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

176. MHESHIMIWA HAROUS SAID SULEIMAN (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kiwanda cha Makonyo Wawi kinakabiliwa na uchakavu wa mitambo pamoja na uchakavu wa vinu vidogo vidogo vya kuzalisha mafuta ya mimea vilivyopo katika maeneo ya Mgelema, Mbiji, Kengeja, Mjimbini na Mtakata.

(a) Je, kuendela kutumia mitambo chakavu kunaleta tija inayokusudiwa katika uzalishaji wa mafuta.

(b) Je, kuna sababu gani zinazopelekea Shirika kushindwa kumudu gharama za kuitengeneza mitambo yake.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

50. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Zanzibar ni nchi ya visiwa inayotegemea bahari yake kwa chakula na kutoa ajira kwa wananchi wake. Hata hivyo, sekta hiyo inakabiliwa na changamoto kubwa ya uingizwaji wa samaki wasio na viwango kutoka nje ya nchi.

(a) Kwa nini Serikali haipigi marufuku uingizaji wa samaki kutoka nje kuuzwa Zanzibar.

(b) Je, Zanzibar inamahitaji ya tani ngapi za samaki kwa mwaka na uwezo wa wavuvi wetu ni kuvua tani ngapi kwa mwaka.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

166. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi)-

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika kuimarisha utoaji wa huduma za elimu kwa wananchi, Serikali imejiimarisha kwa kujenga skuli mbalimbali ikiwa ni njia moja ya kuyaenzi Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964. Pamoja na kujengwa kwa majengo mengi kwa ajili ya kuwapatia watoto wetu elimu, changamoto ya uwepo wa walimu imekuwa ikiongezeka siku hadi siku hasa kutokana na walimu wengi kustaafu.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza idadi ya walimu wenye sifa ili kuondosha tatizo la uhaba wa walimu ambapo kwa sasa uwiano uliopo katika Wilaya ya Chake Chake ni wastani wa wanafunzi 100 kwa mwalimu mmoja.

(b) Ili kuongeza kiwango cha ufaulu ni pamoja na upatikanaji wa vifaa vya kufundishia hasa vifaa vya maabara kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi. Je, ni lini tatizo la uhaba wa vifaa hivyo katika skuli ya Wawi litatatuliwa ili kuondoa changamoto ya kufeli kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

157. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni)-

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na wimbi kubwa la ubomoaji na kujengwa upya nyumba za makaazi ya watu katika maeneo mbali mbali ya visiwa vya Unguja na Pemba. Hata hivyo, ujenzi huo umekuwa hauzingatii Sheria za ujenzi kwa baadhi ya watu kujiongezea maeneo tofauti na ilivyokuwa jengo la awali linalobomolewa, hali inayopelekea kuzibwa kwa baadhi ya njia kubwa au vichochoro kuwa finyu.

(a) Je, kwanini Serikali haiweki mfumo maalumu wa kufuatilia kwa karibu ujenzi wa aina hiyo kwa kutumia Masheha na Madiwani wa maeneo husika.

(b) Je, kwanini watu wanaachiwa toka wanabomoa jengo la awali mpaka wanajenga upya au kukarabati bila ya kuchukuliwa hatua zozote za kudhibiti uharibifu wa mipango miji.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kwa mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,**
**27 Mei, 2021.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**